



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO KWA WANANCHI WA MKOA WA DAR ES SALAAM KUHUSU
KUJIANDIKISHA KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA MPIGA KURA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inapenda kuwatangazia wananchi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam wenye sifa za kujiandikisha kuwa wapiga kura, kujitokeza katika vituo vya kujiandikishia. Zoezi hili lilianza siku ya Jumatatu tarehe 17 Machi, 2025 na linatarajiwa kukamilika siku ya Jumapili tarehe 23 Machi, 2025.

Uboreshaji utahusisha:-

1. Kuandikisha Wapiga Kura wavya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi.
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100.

TUME INAWAKUMBUSHA WANANCHI WOTE WA MKOA WA DAR ES SALAAM KUWA WAPIGA KURA WALIOJIANDIKISHA MWAKA 2015 NA 2020 NA AMBAO KADI ZAO ZA MPIGA KURA HAZIJAPOTEA AU KUHARIBIKA AU HAWAJAHAMA KUTOKA ENEO WALIOJIANDIKISHA MWAKA 2015 NA 2020 HAWATAHUSIKA NA ZOEZI HIVYO WASIENDE KATIKA VITUO VYA KUANDIKISHA WAPIGA KURA.

Imetolewa leo tarehe 19 Machi, 2025 na:

Kailima R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI